

UTEUZI WA MRAJIS WA MAHKAMA KUU

Tume ya Utumishi ya Mahkama imefanya uteuzi wa Mrajis wa Mahkama Kuu na Manaibu Warajis wawili wa Mahkama.

Mhe. Mohamed Ali Mohamed ameteuliwa kuwa Mrajis na Mhe. Hussein Makame Hussein na Mhe. Salum Hassan Bakar kuwa Manaibu Warajis wa Mahkama Kuu

Akitoa taarifa hiyo katibu wa Tume ya hiyo Mhe. Ali Ameir Haji amesema uteuzi huo umefuatia kikao cha Tume na umeanza rasmi mara moja

Mhe. Mohamed Ali Mohamed kabla ya uteuzi huo alikuwa Hakimu wa Mahkama ya Mkoa Mwera na Mhe. Hussein Makame Hussein alikuwa Mrajis wa Jimbo Pemba wakati Mhe. Salum Hassan Bakar alikuwa Makamo Mwenyekiti wa Mahkama ya Ardhi Pemba.